# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA
# MTIHANI WA KUHITIMU KIDATO CHA SITA

**121/1** **KISWAHILI 1**

(Kwa watahiniwa Walioko na Wasiokuwa Shuleni)

**Muda: Saa 3** **Mwaka: 2022**

**Maelekezo**

1. Karatasi hii ina sehemu A na B zenye jumla ya maswali **nane (8)**.
2. Jibu maswali yote katika sehemu A na maswali **matatu (3)** kutoka sehemu B. Swali la **nane (8)** ni la lazima.
3. Sehemu A ina alama **arobaini (40)** na sehemu B in alama **sitini (60)**.
4. Zingatia maagizo ya **kila sehemu** na ya **kila swali**.
5. Simu za mkononi na vitu vyote visivyoruhusiwa **havitakiwi** katika chumba cha mtihani.
6. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

2 202121 100012

## SEHEMU A (Alama 40)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

1. Soma kifungu cha habari kifuatacho kwa makini kisha jibu maswali yanayofuata:

Uhuru ni ua lisilonyauka, lenye umbo zuri limtialo kiumbe yeyote furaha. Kasuku akinyimwa uhuru huweza kusahau ufundi wake wa kuimba, hudhoofu na hatimaye hufa kwa **kihoro**. Halikadhalika, mtoto mchanga hupiga mateke na kulia anapoogeshwa, anapovishwa nguo na hata anapolishwa, hayo yote huyafanya ilimradi tu aachwe huru.

Katika nchi yenye **demokrasia** mtu binafsi anayo haki ya kuishi bila kubughudhiwa au kunyanyaswa kwa namna yoyote na mtu, kikundi cha watu au serikali. Mtu ana uhuru wa kwenda apendapo ili mradi asivunje sheria au kuingilia uhuru wa mtu mwingine. Mtu ana uhuru wa kushiriki katika majadiliano na kutoa maamuzi ya mambo yanayohusu mustakabali wa nchi au anaweza kuwakilishwa katika majadiliano na utoaji wa maamuzi hayo na wananchi wenzake. Mwananchi anao uhuru wa kufanya mawasiliano yaliyo halali ili mradi hatoi matamko ya kuzuru mtu au kikundi cha watu. Aidha, mawasiliano yanayoruhusiwa ni yale yasiyo na hali ya uchochezi au ushawishi kwa watu. Mawasiliano hayo yasiwe yanayoweza kusababisha watu kwenda kinyume na matakwa ya uongozi. Mzalendo yeyote anapaswa kuwa na moyo thabiti na hapaswi kusita anapokuwa na dukuduku lolote halali. Vilevile hapaswi **kutaharuki** inapolazimika yeye kukosolewa.

Katika nchi yenye demokrasia ya kweli, serikali hufanya jukumu la kulinda utu wa raia wake. Aidha, serikali hutoa elimu kwa watu wake ili kuwajengea misingi bora ya kujitegemea itakayowawezesha kujenga uchumi. Serikali ikisimamia misingi ya utawala bora wananchi huwa tayari kulihudumia taifa lao kwa moyo wote bila **kinyongo**, kwa sababu juhudi za serikali zinaonekana wazi.

Serikali yoyote yenye kujali utu wa raia wake, husimamia misingi ya demokrasia na haki za binadamu hivyo raia wake huishi kwa amani na ndipo maana halisi ya uhuru inapojidhihirisha. Uhuru ni kitu chenye thamani ambacho hakiwezi kufananishwa na rangi ya nguo, wala ladha ya chakula na hakuna kitu chochote ulimwenguni kinachoweza kuwa na thamani inayoweza kufananishwa na uhuru. Shime wananchi wa nchi za Afrika tuungane pamoja katika kulinda nchi zetu na kuhakikisha kuwa hakuna hali yoyote ya kutawaliwa kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni ili kila nchi iwe na uhuru wa kweli.

**Maswali**

(a) Andika kichwa cha habari kisichozidi maneno matatu.

(b) Orodhesha mawazo makuu matatu yanayopatikana katika aya ya pili.

(c) Taja faida moja ya serikali kusimamia utawala bora.

(d) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika kifungu cha habari.

   (i) Kihoro
   
   (ii) Demokrasia
   
   (iii) Kutaharuki
   
   (iv) Kinyongo

2. Eleza mambo muhimu matano yanayoweza kumsaidia mtumiaji wa lugha kuwa mahiri.

3. Kwa kutumia mifano, fafanua dhana zifuatazo:

   (i) Utata katika lugha
   
   (ii) Rejesta
   
   (iii) Simo (misimu)
   
   (iv) Umahiri wa lugha

4. Bainisha dhima ya kila mofimu iliyopigiwa mstari katika maneno yafuatayo:

   (i) <u>M</u>kimbizi
   
   (ii) <u>Hu</u>nung'unika
   
   (iii) Asi<u>ye</u>ridhika
   
   (iv) Watembea<u>o</u>
   
   (v) Ame<u>ni</u>alika
   
   (vi) <u>Ni</u>mekufikia
   
   (vii) Tume<u>ji</u>takia
   
   (viii) Wata<u>m</u>furahisha
   
   (ix) Pang<u>u</u>a

**SEHEMU B (Alama 60)**

Jibu maswali **matatu (3)** katoka sehemu hii. Swali la **nane (8)** ni la lazima.

5. Jina lako ni Malingumu Sulubu S.L.P 1000 Magu. Andika barua ya kukiri kupokea bidhaa ulizoagiza toka kampuni ya Mchumi Traders wa S.L.P 750 Mwanza. Bidhaa hizo ni jozi 50 za viatu vya ngozi, jozi 100 za soski nyeupe, dazeni 100 za penseli, katoni 100 za sabuni ya mbuni na seti 150 za vikombe vya plastiki.

6. Kwa kutumia hoja sita, fafanua mchango wa serikali katika kukuza Kiswahili nchini Tanzania baada ya uhuru.

7. Kwa kutumia hoja tatu, jadili dai kuwa asili ya Kiswahili ni Kiarabu kisha tumia hoja tatu kuonesha udhaifu wa dai hilo.

8. (a) Taja tofauti tano zilizopo kati ya tafsiri ya kimawasiliano na tafsiri ya kisemantiki.

(b) Tafsiri sentensi zifuatazo katika lugha ya Kiingereza kwa kuzingatia tafsiri ya kisemantiki.

(i) Zawadi anacheza netiboli/mpira wa pete.

(ii) Mama huenda sokoni kila jumamosi/kila jumamosi mama huenda sokoni.

(iii) Anajua chanzo cha maradhi yake/ugonjwa wake.

(iv) Shangazi yangu/mama mdogo wangu atapika chapati tamu.

(v) Ninapendelea/ninapenda kusoma riwaya za Kiswahili.

(vi) Walimu wanafanya kazi nzuri sana.

(vii) Mkutano wa wiki tatu/majuma matatu unakwisha/utakwisha/utafungwa leo.

(viii) Kama watashinda watapewa zawadi/tuzo.

(ix) Ulisikia lakini hukutaka kujibu/kuitika.

(x) Usiende, labda kama una/labda uwe na sababu ya msingi.